JINA …… NAMBA YA MTIHANI ……

JINA LA SHULE ……

102/2
KISWAHILI
KARATASI YA 2
Lugha
2018
Saa 2 ½

(Hati ya kuhitimu elimu ya sekondari Kenya (K.C.S.E)

- Andika jina na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu
- Jibu maswali yote. Majibu yako yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
	Jumla	

Karatasi hii ina kurasa11Hakikisha kuwa karatasi zote zimechapwa
Jibu maswali yote kulingana na maagizo

UFAHAMU

Soma makala haya kisha ujibu maswali

Waswahili wanasema kuwa mbiu ya mgambo ikilia kuna jambo. Wanasayansi wamekuwa wakitoa habari za kuhuzunisha kuhusu hali joto ulimwenguni. Uchunguzi wao unabainisha kuwa kiwango cha hali joto kinazidi kupanda. Hii inaonyesha kuwa mazingara yetu yanazidi kupoteza unyevu na badala yake hali ya ukavu inashamiri. Hali hii inatia wasiwasi mno. Ulimwengu mzima sasa unajitahidi kuyatilia mkazo mazingira kwa kuwataka watu wote kuyahifadhi na kuyarejesha katika hali yake ya awali.

Katika mataifa yanayoendelea, watu hukata miti na kuchoma makaa kama njia ya kupata kawi iliyo muhimu katika shughuli za uandaaji wa mila. Wengine hukata miti kusudi wapate kuni. Wengine nao hukata miti ili waweze kupasua mbao za kujenga na pia kutengeneza samani na vifaa vinginevyo. Haja za miti si haba. Pamoja na kwamba haja hizi ni lazima kutimizwa, miti imekuwa ikikatwa tu bila kujali viwango vya ukataji huo au kupanda mingine kuziba pengo la ile iliyokatwa. Matokeo yake ni watu wachache walafi kujitajirisha ilhali kizazi kizima kinaangamia. Ukataji miti huivua ardhi na kuiacha uchi. Mvua inaponyesha udongo wenye rutuba husombwa na kupelekwa baharini. Vilevile ukosefu huu wa miti unamaanisha kuwa unyevunyevu ulio muhimu katika hatima ya kuleta mvua haupo. Mavuno yake ni kiangazi. Ukame, njaa, jangwa na maangamizi. Tayari tumeshuhudia hapa nchini mwetu jinsi vipindi vya ukame vinazidi kuwa virefu kuliko awali. Kwa mara kadha sasa tumekuwa na mgao wa umeme kwa vipimo, mgao wa maji kwa vipimo na kadhalika. Hizi zote ni athari za kutoyajali mazingira yetu.

Sehemu za ulimwengu zilizoendelea kiteknologia zina matatizo ya aina yake. Ongezeko la magari na viwanda katika nchi hizo sasa vimeanza kuwatia wenyewe joto. Magari yanatoa mioshi iliyo hatari kwa afya ya watu na mazingira kwa jumla. Katika baadhi ya miji ya nchi hizo zilizoendelea, vimerekodiwa visa vya maji meusi tititi ya mvua. Kisa na maana ni kwamba wamezichafua anga zao kupitia mioshi itokayo viwandani na kwenye magari. Maji hayo si salama kwa matumizi ya binadamu wala mimea na wanyama. Katika baadhi ya miji wingu jeusi huwa limetanda utadhani ni giza lililoingia majira ya adhuhuri. Ni hayo sasa yamebuni sheria kali ambazo zinalenga kuyaokoa mazingira yao.

Nchi nyingi ulimwenguni zimeandika na kutia sahihi mikataba ambayo inapiga vita kutumiwa mafuta ya risasi na kuanza kutumia isiyo ya risasi. Nchi nyingi sasa zanaelekea kutupilia mbali matumizi ya petroli au diseli ya risasi na kuanza kutumia isiyo ya risasi. Wataalamu wanasayansi wamebaini kuwa mafuta ya risasi yana athari mbaya kwa mazingira. Yenyewe ni tishio kwa afya ya mwanadamu.

Katika sekta ya mazao na kilimo, wanasayansi walipoona kuwa ulimwengu ulikuwa unakabiliwa na tishio la njaa kufuatia uhaba wa chakula, hawakusita kubuni mbinu mpya za kuzidisha mazao. Mojawapo na hii ni ya awali kabisa, ni kutumia mbolea zilizotengenezwa viwandani kuiongezea ardhi rutuba. Uvumbuzi wa baadaye umeonyesha kwamba mbolea hizi zina kemikali ambazo hufyonzwa na mimea ya chakula. Mimea hii inapokomaa na kuanza kutumiwa na mwanadamu kama chakula, humletea madhara katika afya yake. Baadhi ya kemikali hizo, hukokotwa hadi kwenye maziwa na bahari zetu ambamo muna samaki. Samaki hawa, mbali na kuathiriwa na kemikali hizo hatimaye huingia katika mwili wa mwanadamu na kuanza kuitatiza afya yake.

Hapana shaka kwamba ulimwengu wetu umeendelezwa na kukomazwa na teknolojia. Lakini pia ulimwengu uu huu umetishiwa na teknolojia. Teknolojia na maendeleo ni wakala wakubwa wa ongezeko la hali ya joto duniani. Iwapo hali hii huitasitishwa mwanadamu atajikuta katika mazingira ya taabu na dhiki za kumwangamiza kabisa.

Maswali

a) Kwa nini ulimwengu unajitahidi kuyahifadhi mazingira? (Alama 2)

Eleza matatizo matatu ya kimazingira yanayokabili nchi zilizoendelea (Alama 3)

Kwa Mujibu wa kifungu ulichosoma , eleza hasara ziletwazo na ukataji wa miti . (Alama 4)

d) Taja methali mbili zinazotumia maneno yafuatayo (Alama 2)

i) Miti……

e) Mvua kifungu eleza maana ya : (alama 4)

i) Wakala ……

ii) Kawi……

iii) Mafuta ya risasi……

iv) Inashamiri ……

UFUPISHO

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Ukiwa mtoto unadhani ulimwengu ni kipande kimoja cha keki kilicho kitamu mithili ya asali. Hakuna dhiki, hakuna mateso, hakuna kuhuzunika kwa aina yoyote. Neno huzuni linasikika masikioni kama neno lisiloelekea kwenye uhalisia wowote. Kwa watoto, dunia imejaa raha, starehe na vicheko visivyoisha. Maisha ni ahadi njema, yenye matokeo ya kufurahisha na kustarehesha tu, sio kudhikisha na kuhuzunisha.

Huyu tunayemzungunizia hapa ni mtoto mdogo ambaye hajajua kubainisha kitendekacho mkono wake wa kushoto na kile kinachofanyika hasa katika mkono wake wa kulia. Hata hivyo, jinsi mtoto anavyoendelea kukua na kufahamikiwa na mambo, vigambo na kadhia zinazoendelea katika mazingira yake, anabainikiwa na mengi machungu ambayo huleta huzuni, sio raha.

Hebu tuanze na nyumbani kwao mtoto. Aghalabu, watoto wote hupendwa kwao nyumbani, iwapo wazazi wao ni watu waungwana, na wana nafasi ya kulea watoto wao bila taabu. Hata hivyo watoto huchapwa pale wanapokuwa watundu, jambo ambalo huwahuzunisha sana, japo ni wajibu wa wazazi sababu, kama isemwavyo, mcha mwana kulia hulia yeye. Pili, inajulikana wazi kwamba watoto wengi siku hizi huenda shule. Huko shule, wao hupendelea sana kucheza kuliko kusoma. Ili wasome kama inavyotakikana, ni sharti waelekezwe barabara katika njia hiyo na walimu wao. Katika kuelekezwa huku, walimu wanaweza kulazimika kuwaadhibu, hasa wale watoto ambao huzembea na kutofanya kazi zao wanazopewa kufanya nyumbani kama kawaida ya mfumo wa shule ilivyo. Watoto wa aina hii wanapotiwa adabu raha hujitenga na huzuni kuwatawala.

Huzuni, hivyo basi, inaonekana ya kuwa ni uso wa pili katika maisha ya mwanadamu, uso wa kwanza ukiwa raha. Na kwa hakika wanaohuzunika si watoto peke yao. Kila mtu duniani ni sharti, katika wakati mmoja au mwingine, azongwe na huzuni. Inajulikana wazi kwamba wanadamu wote hawapendi huzuni asilani na hakika kabisa, kila binadamu huchukia huzuni na kustahabu raha. Hata hivyo, raha humjia binadamu kwa nadra sana, ilhali huzuni humvamia wakati wowote, hata akiwa yumo katikati ya kustarehe. Si tu, inajulikana dhahiri shahiri kwamba hakuna mtu asiyewahi kuonja huzuni, japo wapo watu wengi kwelikweli wasiowahi kuonja raha maishani mwao.

Zingatia mtoto anayezaliwa, halafu wazazi wake wanaaga dunia, pengine katika ajali, kabla mtoto mwenyewe hajaweza kujikimu. Mtoto huyu anaishi kutegemea jamaa za wazazi wake. Watu hawa wasipokuwa na nafasi wao wenyewe kimaisha pamoja na ukarimu unaohitajika basi mtoto anateseka na kuhuzunika sana katika maisha yake yote. Ama zingatia mtoto anayetupwa na mamake kijana, aliyempata bila kupanga. Hata mtoto huyu akiokotwa na kulelewa na wahisani, maisha yake yatakuwa ya taabu, dhiki na huzuni. Au zingatia mtoto anayelelewa na mama wa kambo anayeondokea kuwa mwovu. Mtoto huyu atakayoijua ni huzuni tu. Ama zingatia mtoto ambaye babake ni mlevi na analojua ni kurudi nyumbani usiku akiimba nyimbo za kilevi, kuita mkewe kwa sauti kubwa, kuitisha chakula na kufurahia kupiga watoto wote na mama yao ndipo apate usingizi mnono. Mtoto mwenye baba wa aina hiyo atakayoijua ni huzuni tu, si raha asilani.

a) Bila kubadili maana, fupisha aya nne za mwanzo.(Maneno 90- 100) (alama 10)

Matayarisho

……

Jibu

b. Ukizingatia aya ya mwisho , eleza hali mbalimbali zinazowatia watoto huzuni (Alama 2)
(Maneno 20-25)

Matayarisho

……

Jibu

……

3. <u>MATUMIZI YA LUGHA</u>

A) Akifisha

Una kiberiti Yule mtu aliniuliza na nilipotoa kiberiti na kawasha yule mtu alinizaba kofi maria alieleza (alama 3)

……

b) Taja sauti nne za konsonanti ambazo ni za nazali. (alama 2)

……

c) Tunga sentensi inayodhihirisha matumizi ya ngeli ya I- Zi

Umoja …… (alama 2)

Wingi……

b) Tunga sentensi ya neno moja yenye mofimu zifuatazo . (alama 2)

i) Nafsi ya tatu umoja ……

ii hali timilifu……..

ii) Kitendwa …….

iii) Mzizi…….

iv) Kiishio……

c) **Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia jedwali** (alama 3)

Sikumwadhibu kwa sababu alikuwa mgonjwa .

……

f) Neno mlevi limetumikaje katika sentensi zifuatazo ? (alama 2)

iii) Mlevi alisababisha ugomvi ……

v) Mtu mlevi alisababisha ugomvi ……..

g) Bainisha kishazi huru na kishazi tegemezi katika sentensi hii. (alama 2)

Nitaenda nyumbani ingawa ninaumwa na kichwa

……

h) Tunga sentensi sahihi ukitumia **hadi** kama (alama 2)

Kihusishi cha wakati ……

ii) Kihusishi cha mahali (alama 2)

Eleza matumizi ya kwa, ku, ka katika sentensi hizi . (alama 3)

i) Nitakutaka ufike hapa

ii) Kachezeni kule nje

iii) Yule mtaalamu alielezea maana ya utandawazi kwa ufasaha .

Ziandike sentensi zifuatazo ukizingatia maagizo. (Alama 2)

i) Chakula kinachoiva vizuri ndicho kinacholiwa (hali ya mazoea)

ii) Timu ile imeshinda . Haikucheza vizuri (Tumia ijapokuwa)

Sentensi hizi ni za aina gani? (Alama 2)

i) Mkulima aliyekata rufani atasaidiwa kesho .

Walimu na wazazi wanatengeneza bweni .

j) **Andika kinyume cha**

i) Mtweke Bi. Kizee mtungi huu wa maji . (alama 2)

ii) Mama alitandaza zulia kubwa sebuleni .

m. Tumia vitenzi - nya na ja kutunga sentensi sahihi katika kauli ya kutendewa (alama 2)

i……

ii)……

n. **Andika kwa msemo halisi**

Wanga alisema kuwa alikuwa amepata alama zote katika mtihani wa mwisho wa mwaka

(alama 2)

o) **Andika kwa wastani halafu kwa ukubwa .**

Kibuzi kile kinono kina kiguu kinachouma . (alama 2)

i)……

ii)……

p) **Andika kwa wingi .**

Kuku yuyu huyu ndiye aliyetaga yai hili . (alama 2)

q) **Yakinisha sentensi hii .**

Usipolala sana hutapona haraka. (alama 1)

w) **Tunga sentensi kwa kutumia maneno yafuatayo ili kubainisha maana** (alama 2)

i) Bana

ii) pana

4. **ISIMU JAMII**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata

Nini? Umetumana ?

Utatumia chai ya kahawa au majani?

Nataka kachai na katosti!

Tosti ni kumi . Tea is twenty shillings

Mbona unaniletea maji ukisema ni chai ?

Samahani customer . Ngoja nikuletee moto .

a) Lugha iliyo katika kifungu hiki hutumika katika muktadha upi? (Alama 1)

……

b) Taja sifa nne za matumizi ya lugha katika muktadha huu. (Alama 4)

c) Toa sababu mbili zonazoonyesha umuhimu wa lugha ya Kiswahili nchini Kenya

d) Orodhesha hatua tatu zinazoweza kuchukuliwa kusuluhisha matatizo yanayokumba Kiswahili nchini Kenya (alama 3)